WCB
Workers Compensation
Board of Manitoba

Bima na Faida

Ikiwa utaumia
ukiwa kazini,
tupo hapa
ili kukusaidia.

Ikiwa utaumia ukiwa kazini, tupo hapa ili kukusaidia.

wcb.mb.ca

Chapisho hili linatolewa kwa taarifa ya jumla pekee.
The Workers Compensation Act (Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi)
wa Manitoba na Kanuni, na sera za bima ya WCB ndiyo mamlaka
ya mwisho kwa usimamizi wa bima na madai.

Bima na Faida

Hakuna anayetarajia kuumia kazini, lakini kila mara majeraha ya kazini hutokea. Hata hivyo, bima ya WCB yapo kwa ajili yako. Kama utaumia kazini, tambua kwamba una bima unayohitaji.

Mwajiri wako analipia malipo yote kuhakikisha unalipia kila kituuna bima unapoumia kazini. Mwajiri wako lazima akulipe siku nzima kwa siku utakayoumia kazini, sio tu mpaka muda ulioumia.

Bima ya WCB inalipa sehemu ya mshahara wako na kulipia gharama za matibabu yako kama umeumizwa kazini.

Ni Nini Bima ya WCB wanalipia?

Hapo chini ni baadhi ya faida zinazopatikana kwa wafanyakazi walioumia. Kwa taarifa maalumu kama unaweza kulipiwa chochote kati ya yafuatayo, ongea na mtu wako wa WCB.

- **kupoteza mshahara**
- **huduma ya matibabu na gharama za dawa**
- **matibabu ya meno**
- **chiropractic au matibabu ya physiotherapy**
- **huduma za likizo za kupona**
- **malipo ya mkupuo kwa ajili ya ulemavu wa kudumu**
- **pensheni**
- **faida baada ya kifo**

Kupoteza mishahara

- Bima ya WCB wanaanza kukulipa mshara uliopoteza siku ya kazi inayofuata baada ya kuumia.
- Unapokea asilimia 90% ya mshahara ulipaswa kupata. Kwa baadhi ya kesi mshahara unaopeteza unaweza kulipwa asilimia 100% ya mshahara unaopata sawa na asilimia 100% ya kiwango cha chini kwa mwaka kilichopangwa na WCB. Kwa taarifa zaidi soma nakala ya ukweli kuhusu Muongozo wa Faida inapatikana kwenye wcb.mb.ca.
- Tuna hesabu asilimia 90% au 100% kamili (kiwango cha kwenda nacho nyumbani) kwa kuchukua mapato yako na kutoa makato, kama vile ushuru, CPP na EI. Makato ya ushuru yanalingana na hadhi yako ya kuolewa na idadi ya watu wanaokutegemea. Faida yako pia inaweza kuathiriwa na mambo mengine kama muda za ziada kazini, bonasi, kusimamishwa mara kwa mara au mara kadhaa, na mapato kutoka vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na kujiajiri.
- Faida za bima ya WCB hazina ushuru; kwa hiyo, tunakata kiwango sawa cha ushuru ungepaswa kupata.
- Mwisho, kama una bima nyingine ambayo itakulipia wakati haupo kazini, kiwango chochote unachopokea zaidi ya asilimia 100% ya kiwango chako kamili unachopoteza kwenye kiwango chako **kitakatwa** kutoka unachopata kutoka WCB. Ni wajibu wako kumjulisha mtu wako wa WCB kuhusu malipo yako ya ziada.

Gharama Zingine

Unapoumia kazini, unahitaji kwenda hospitalini au kuomba dawa.

Kama gharama hizi zinaungana pamoja katika sehemu yako ya kazi ulipoumia, wanaweza kulipiwa na WCB. Wasiliana na mtu wako wa WCB kujua kama malipo yatalipiwa na bima ya WCB.

Malipo ya gharama za matibabu ni pamoja na:

- gharama za hospitali
- dawa (pamoja na dawa za kuandikiwa)
- matibabu ya meno
- viungo vya bandia, vitu vya kushikilia mwili, magongo, fimbo, msaada wa kusikia na misaada mingine
- orthotics au viatu
- kubadilisha au kutengeneza prosthetics, miwani au meno ya bandia kama yameharibika
- kubadilisha nguo za kazi kama zimeharibika ulipoumia kazini
- usafiri na posho kama unapaswa kusafiri kwa matibabu

Malipo ya Kudumu ya Kuharibika

Unaweza kupewa malipo yote mara moja, pamoja na mshahara utakaopoteza, kama umepata ulemavu wa kudumu kwa sababu ya kazi.

Malipo yanazingatia upotevu wa kazi yoyote uliosababishwa na ulemavu.

Huduma Nyingine Zinapatikana WCB

Rudi kwenye Huduma ya Kazi

Bima ya WCB watafanyakazi na wewe kuhakikisha unapata msaada unaohitaji kurudi kazini. Kurudi kazini ni mpango wa hatua unaokujumuisha na mtoa huduma ya afya, pamoja na mwajiri wako, na kwa baadhi ya hali mwakilishi wa umoja wako. Kazini wanaweza kuwa na programu za kurudi kazini tayari.

Huduma ya Likizo ya Kupona

Kama hautaweza kufanyakazi ulipoumizwa kwa mwajiri wako kutokana na athari za kuumia, unaweza kustahili huduma ya likizo ya kupona kupitia bima ya WCB.

Likizo ya inakusaidia kurudi kwa mwajiri anayeheshimu uwezo wa kazi yako. Hii ikiwa ni pamoja na kukusaidia kutafuta kazi mbadala katika huduma tofauti tofauti kufanyakazi kwa kuajiriwa tena mpaka kufundishwa upya.

Wajibu wa Kuajiriwa

Mnamo Januari 1, 2007, Sheria inawataka waajiri ambao wana masaa 25 au kuajiriwa au kazi ya muda kuajiriwa upya wafanyakazi majeruhi ambao alikuwa amewaajiri kwa angalau miezi 12 mfululizo kabla ya kujeruhiwa. Kwa taarifa zaidi tembelea **wcb.mb.ca** au piga simu **204-954-4321** au piga simu bure **1-855-954-4321** kupata nakala ya *Wajibu wa Kuajiriwa.*

Utendaji wa Haki ofisini

Utendaji wa Haki Ofisini ni ofisi inayojitegemea inayofanyakazi kuhakikisha kuna utendaji wa kazi WCB. Ofisi inafanyakazi kama Ombudsman kwa ajili wafanyakazi waliojeruhiwa, wategemezi wao, na waajiri kutatua masuala wanaweza kuwa nayo na WCB, wakati huo huo wakiwasaidia WCB kuboresha ubora wake wa huduma. Wanaweza kupatikana kwenye **204-954-4467** au piga simu bure **1-855-954-4321**.

Kuomba Kopi ya Mafaili

Unaweza kuomba nakala ya kufaili malalamiko baada ya bima ya WCB kufanya maamuzi yao ya mwanzo ya kukubali au kukataa malalamiko. Muulize mtu wako wa WCB au piga simu katika Idara yetu ya Kuangalia Faili kwenye 204-954-4453. Mwajiri na Mwanasheria pia anaweza kuomba nakala ya mafaili. Nakala za faili za mwanzo ni bure.

Rufaa

Kama unataka kukata rufaa ya maamuzi yaliyofanywa ya malalamiko yako WCB, jadili maamuzi hayo na mtu wako wa WCB kwanza. Kuna njia mbili rasmi, hatua mbili za kukata rufaa zinapatikana kwako kama bado haukubaliani na maamuzi.

Rufaa ya Kwanza ni Ofisi ya Mapitio. Mara utumapo *Maombi ya Mapitio* kutoka (inapatikana kwenye wcb.mb.ca) Ofisa wa Mapitio atapangwa kufikiria rufaa yako.

Kama bado haujaridhika na maamuzi, unaweza kukata rufaa katika Tume ya Rufaa, ambayo ni kiwango cha mwisho cha rufaa. Unaweza kukata rufaa kwa maandishi au kuzungumza na mtu kwenye bodi ya watu watatu inayowakilisha wafanyakazi, waajiri, na umma. Rufaa inaweza kuwekwa mbele na wewe, kama utapenda, mwakilishi wako.

Kama unahitaji msaada kufanya rufaa katika Ofisi ya Mapitio au Tume ya Rufaa, unaweza kuwasiliana na Ofisi ya Mshauri wa Wafanyakazi. Ofisi ya Mshauri wa Wafanyakazi anaweza pia kukupatia ushauri na/au mbadala binafsi kuhusiana na mambo au uamuzi wa WCB.

Worker Advisor Office (Ofisi ya Mshauri wa Wafanyakazi)
406 – 401 York Avenue
Winnipeg, MB R3C 0P8
Simu 204-945-5787
Nukushi 204-948-2020

Taarifa za ujumla za WCB

- Mwajiri wako hulipia faida zote za bima ya WCB – haziondolewi kwenye malipo yako wala kufadhiliwa na dola za ushuru.
- Bima ya WCB inaendeshwa na Halmashauri ya Wakurugenzi inayojumuisha Mwenyeketi wa Bodi asiyeegemea upande wowote, waakilishi watatu wa wafanyakazi, waakilishi watatu wa waajiri na waakilishi watatu wa maslahi ya umma.
- Bima ya WCB imejitolea kutoa huduma ya haraka, rahisi, ya kujali, ya haki na wazi.
- Una haki ya kulalamika WCB kama umeumia kazini. Ni kinyume na sheria kuombwa na mwajiri wako kutofaili malalamiko.

WCB
Workers Compensation Board of Manitoba

Mshirika wa kuaminika, anayehakikisha leo na kujenga kesho iliyo salama.

Ikiwa utaumia ukiwa kazini, tupo hapa ili kukusaidia.

Namna ya Kutufikia

Workers Compensation Board of Manitoba
333 Broadway, Winnipeg, MB R3C 4W3

Tutumie barua pepe
wcb@wcb.mb.ca

Kwa taarifa zaidi, tembelea
www.wcb.mb.ca

au tupigie simu
204-954-4321

au simu bila malipo
1-855-954-4321

Ripoti udanganyifu au uzembe

Piga simu 204-888-8081
au piga simu bure 1-844-888-8081
Barua pepe **Compliance@wcb.mb.ca**

Kazi SALAMA ni jukumu la kila mmoja. Kuzuia majeraha ni vizuri kwa waajiri na wafanyakazi. Kwa maelezo zaidi, tembelea kwenye:

safemanitoba.com

au piga simu 204-957-SAFE (7233)
ndani ya Winnipeg
au 1-855-957-SAFE (7233) nje ya Winnipeg

SAFE WORK MANITOBA

WCB1001E-27/11/14 SWAHILI

CEP SCEP UNION LABEL